MACHOZI YA FURAHA

Hadithi za Mashujaa na Majitu



Donald Sybertz

MACHOZI YA FURAHA

Hadithi ya Mashujaa na Majitu

Donald Sybertz

Mathews Bookstore & Stationers
P. O. Box. 42067
Dar es Salaam.

Mathews Bookstore & Stationers
P .O. Box 42067
Dar es Salaam.

© Donald Sybertz, 2006

Michoro na: Khalid Yusuf
Mpangilio wa kurasa na: Albert M.Mwaipyana

ISBN 9987 602 39 8

Haki zote zimehifadhiwa.

Utangulizi

Ngano *(Myths)* ni hadithi zinazohusu hamu ya binadamu kwa mambo yanayodumu, hasa hamu ya uzima wa milele. Kuna hamu ya kila binadamu ya kuishi milele.

Ngano hii ya Shing'weng'we na Masala Kulangwa inahusu kifo na ufufuko. Shing'weng'we ambaye anaendelea kutumeza mpaka sasa ni mfano wa kifo. Na tumbo la Shing'weng'we ni mfano wa kaburi.

Hawa walionyakuliwa wakiwa wazima kutoka tumboni mwa Shing'weng'we ni mfano wa waumini wake Kristo, watakaofufuliwa kutoka kaburini wakati atakapokuja Kristo kuangamiza kifo.

Kristo alikishinda kifo msalabani. Lakini maangamizi kamili ni jambo tunalosubiri kwa matumaini.

Kwa hiyo, kifo bado kipo. "Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni kifo," (1Kor 15:26).

"Lakini ukweli ni kwamba Kristo amefufuliwa kutoka wafu kwanza na wale waliolala katika kifo," (1Kor 15: 51 -52 & 1 Kor 15:57).

Napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Utafiti ya Ndoleleji, Shinyanga, Tanzania: George Edward, John Mahona, Justina Deus, Peter Lugandu, Regina Nkanda, Sospeter Mbiyung'he.

Mwisho natoa shukrani kwa padri Joseph Healey na John Mbonde ambao daima walinihimiza kukamilisha uandishi wa kijitabu hiki, hata nitapata nguvu ya kukamilisha hadi kuchapishwa. *Nalung'wa naba.* Methali hii ya Kisukuma inamhusu mtu ambaye hufanana na mbung'o, ang'ang'aniaye bila kuchoka, huku akiendelea kukujia tena na tena na kamwe hakuachilii.

Donald Sybertz
Dar es Salaam, Tanzania
5 Oktoba 2006

SEHEMU YA KWANZA

MAJITU

Hapo zamani, alikuwepo Mzee aliyekuwa na wana saba wa kiume. Kati ya watoto wake hao saba, mmoja wao alikuwa na chongo. Ndiye kitindamimba. Baba yao alifikiria kuwaoza. Siku moja, aliwaita kwenye kikao chake akawaambia, "Wanangu, muende mjini, mkatafute mali za kuolea." Nao wakakubali. Walipokubali, aliwaambia tena, "Katika safari yenu mtembee hadi njia pana. Mkifika pale, mtakuta njia mbili, nyembamba na ngumu. Na nyingine ni pana na rahisi. Piteni njia nyembamba na muache ile pana."

Walipofika kwenye njiapanda aliyoisema baba yao, kitindamimba mwenye chongo akawaambia, "Wakubwa zangu, tupite njia nyembamba jinsi baba alivyotuagiza."



Lakini kaka zake walikataa, wakasema, "Hapana sisi hatupiti njia nyembamba. Ni mbaya mno, na tena ina harufu mbaya mno. Kama unapenda, nenda wewe mwenyewe na chongo lako."

Kitindamimba huyo mwenye chongo, akakosa la kufanya, akajilazimisha kuwafuata kwa shingo upande. Akaenda nao hivyohivyo.

Wakafuata wote njia pana. Walitembea safari ndefu. Mwisho, wakafika katika kijiji kimoja. Wakawakuta wasichana saba. Mdogo wa hao wasichana alikuwa na chongo pia. Wasichana hao walipowaona wavulana wale wakija, waliwapokea kwa furaha kubwa mno. Wasichana walisema kwa furaha, "Jamani tumeolewa, tumeolewa." Na papo hapo walijichagulia, kila mmoja na wake wakisema, "Wangu huyu, wangu huyu." Na yule msichana mwenye chongo naye akasema, "Nami nimepata mwenye chongo mwenzangu."

Baada ya kuchaguana huko, wasichana waliwaambia waume zao, "Twendeni sasa nyumbani kwetu mkamsalimie bibi yetu." Wakakubaliana. Kabla hawajafika nyumbani, bibi yao aliwaona kwa mbali kidogo. Walipofika nyumbani aliwauliza, "Vipi wajukuu zangu, mmeolewa?"

Nao wakakubali, "Ndiyo bibi, tumeolewa."

Na mwenye chongo pia akajinadi, "Na mimi bibi, pia nimeolewa na mwenye chongo mwenzangu."



Kulipokuchwa, walienda kulala. Ulipofika usiku wa manane, wake zao waliamka, wakaanza kucheza ngoma. Wakati wa kucheza waliimba hivi:

"Tunakula kirabisirabisi,
Tunakula kirabisirabisi."
(Tunakula cha dezo)

Bibi yao akawaambia, "Na mimi mnibakizie supu na utumbo." (nyama wanayokula akina bibi vizee). Nao wakamjibu, "Bado siku, bado siku" (hawajanenepa).

Kulipokaribia kupambazuka muda wa majogoo kuwika, wasichana hao walisambaa, wakaenda ndani kulala. Kumbe mdogo wa wale wavulana alikuwa macho. Alikuwa akitazama matendo yale ya kichawi. Kulipokucha, aliwaambia kaka zake huku akitetemeka, "Ndugu zangu, hawa wanawake tuliowaoa, siyo watu, ni majitu."

Kaka zake walimbishia, wakamjibu, "Kwenda zako na chongo lako! Unataka utuzuie raha?"

Naye akawajibu, "Mmeyakataa maoni yangu mkinitukana chongo langu siyo? Sawa. Ingawaje nina chongo kweli, lakini kwa nini mnakataa maneno yote ninayowaambia? Basi, hata hivyo, tufanye hivi: leo tukilal nitawaamsha mjionee na kuhakikisha ninyi wenyewe kama mimi ni mdanganyifu. Nitachukua mwiba nimchome aliye karibu na mimi, lakini msishtuke, tutaliwa na majitu hayo. Jiandaeni kuangalia mchezo wa wake zetu jinsi wanavyofanya." Walikubaliana na wazo hilo. Usiku ulipoingia walienda kulala; na saa yao ilipowadia wasichana hao wakaamka, wakaenda kwenye kiwanja chao cha mchezo. Walipofika kwenye kiwanja hicho walianza kucheza na kuimba wimbo wao:

"Tunakula kirabisirabisi,
Tunakula kirabisirabisi,
(Tunakula cha dezo)



Ndipo mvulana mwenye chongo, akamchoma mwiba aliyekuwa karibu naye. Mwisho, wakaamka wote. Kaka zake wakapata nafasi ya kujionea kwa macho yao matendo ya wake zao. Kulipopambazuka mdogo wao aliwauliza, "Vipi

sasa mlikuwa mnanituhumu kuwa mimi ni mdanganyifu, mkinitukana chongo langu, mmejionea wenyewe sasa wanayofanya wake zetu. Bado mnabisha tu?"

Nao wakajibu, "Hapana, tumekubali kabisa. Ulikuwa unasema kweli. Kumbe tulikosea tangu mwanzo tulipoiacha njia nyembamba, ndiyo maana tunapata shida zote hizi."

Mdogo wao akawauliza, "Tufanye nini sasa? Tutafute akili gani ya kuweza kuwatoroka hawa ili turudi nyumbani salama?"

Kaka zake walikuwa hawana la kunena.

Aliwaeleza, "Nitaona mimi njia ya kuturudisha nyumbani salama."

Kaka zake wakamwuliza, "Njia ipi hiyo?"

Naye akawajibu, "Itatubidi tuchonge kinu cha kupaa. Hicho kitaturudisha nyumbani salama na kwa uhakika."

Kaka zake waliafiki, "Ehee, sawa kabisa. Hapo umesema kweli. Kwa hiyo, twendeni tukachonge."

Basi walienda porini, wakaanza kuchonga. Walichonga kwa siku mbili



wakamaliza, wakapanga siku ya kuruka kurudi nyumbani.

Siku ya tatu ilipofika, waliondoka alfajiri, kwenda kwenye kinu chao. Wakakijaribu, kikakubali, kikapaa. Wakati wanajiandaa kuanza safari yao kijana mdogo aliwatahadharisha kaka zake, "Ndugu zangu, punde tu tuingiapo ndani ya kinu, kamwe msithubutu kuangalia nyuma."

Basi, kijana mdogo akaanza kuwaimbia kaka zake kama ifuatavyo:

"Vijana wa kiume tumekwisha,
Tumekwisha, heshima imekwisha,
(Tumeiacha njia, tukamdharau baba).
Dundu-dundu, songa mbele,
Hima unipeleke nyumbani, (kikapaa kwa kasi)
Tumekwisha kaka zangu.
Nilikuwa nawaambia, mwanitukana chongo langu,
Heshima imekwisha, heshima imekwisha."

Alipokuwa akiimba, kinu kikaanza kupaa juu, yeye akiwa dereva. Akaongeza kuimba mpaka kinu kikafika juu kabisa.

Bibi yao hao wasichana alipanda juu ya jabali na aliweza kukiona kinu hicho kinapaa. Aliwaambia wajukuu zake, "Ninyi warembo, nyama hizoo zinaenda hizoo! Zinatokomea."

Waliposikia hivyo, walivaa viatu, wakaanza kukimbia, kuwafuata waume zao. Wanawake hao nao wakatokomea porini. Walipofika katikati ya pori, walijigeuza, wakawa simba.

Wakakimbia kwa nguvu zaidi. Mwisho,

wakakipata kile kinu, wakaanza kukiomba. Kila mmoja akiomba apewe mume wake, akisema, *"We Kinu! Nipe mume wangu, nipe mume wangu."*

Mkubwa wa wale vijana aligeuka, na mara alidondoka, akaliwa na mke wake. Kaka zake wote nao waligeuka nyuma, wakaanguka, wakamalizwa kwa kuliwa na wake zao.

Alibaki yeye peke yake, akiendesha kinu hicho. Hatimaye, aliwasili kijijini kwake. Aliwaona wachungaji, akatua kinu karibu nao, akawaambia, "Mkimwona mwanamke ye yote hapa akiniulizia, tafadhali msimuonyeshe mahali ninapoishi."



Punde si punde, mwanamke huyo alifika kwa hao wachungaji akiwa amejigeuza kuwa binadamu, akawauliza, "Mmemuona mwanaume mmoja akiendesha kinu kinachopaa, anakaa wapi? Wachungaji wakashindwa kufuata maagizo waliyoambiwa, badala yake wakaambizana, 'Mwanamke huyu jinsi alivyo mrembo hivi, kwa nini tuache kumuonyesha? Ikiwa yeye mwenyewe amemchukia au kamchoka, tutamuoa sisi.'

Basi, walimuonyesha njia, akaenda mpaka nyumbani kwa mume wake.

Alipofika aliwakuta wazazi ambao tayari wameshapewa habari na mtoto wao kitindamimba, ya kwamba watoto wao wamekwishaliwa na majitu huko nyikani na ni yeye tu kabaki. Lakini, hata yeye alisema bado alikuwa matatani, kwani mke wake alikuwa akimsaka, ili amle. Aliwasihi sana wazazi wake akisema, "Tafadhali sana, ninawaomba kuwa atakapokuja huyo mwanamke, mpokeeni, lakini katu msimwambie kwamba nipo. Maana huyo siyo mwanamke ni jitu, mwekeni kwenye nyumba nyingine."

Mwanamke yule alipofika, wazazi walifanya kama walivyoambiwa. Walimpokea, wakamweka kwenye nyumba nyingine. Usiku ulipoingia, aliomba mtu mmoja wa kuwa naye ili kumfariji. Wakampa mbwa. Usiku wa manane alitaka kumla huyo mbwa, lakini alishindwa kwani mbwa alikuwa mkali mno. Yule mbwa hatimaye, aliweza kupenya na kutoka nje akichechemea kwenda kwenye nyumba nyingine. Usiku uliofuata alipewa kondoo, akamla. Usiku wa tatu alipewa dume la ng'ombe nalo akalila, akashiba na kuvimbiwa. Akashikwa na usingizi mzito. Basi, mume wake akainuka na kufunga milango yote ya nyumba, halafu aliichoma moto nyumba ile. Mwanamke huyo akateketea humo, yakabaki majivu tu.



SEHEMU YA PILI

BOGA LA AJABU

Ilipoanza kunyesha mvua, liliota boga mahali alipofia huyo mwanamke.Siku moja wasichana wa kijiji kile, walienda kuchuma mboga. Wakaliona boga limeota. Wakaambizana,

"Ona, limeota boga mahali lilipofia lile jitu."

Boga likajibu, "Ona limeota boga mahali lilipofia lile jitu."

Wasichana hao walishangaa mno kulisikia lile boga la ajabu linazungumza. Wakakimbia haraka nyumbani kuwaeleza wazazi wao. "Baba, limeota boga mahali lilipofia lile jitu. Tena, linazungumza kama sisi."

Wazazi nao walikwenda kuangalia mahali ambapo boga limechipuka.

Walilikuta kweli, tena tayari likawa limezaa tunda. Mara lilianza kuwasemesha na kwa mshangao walianza kupiga mayowe. Wanakijiji wengi sana walikimbia kuelekea kwenye tukio hilo, huku wamebeba silaha zao mbalimbali. Umati mkubwa ulijaa tele. Wakakuta boga linazungumza, wakaliambia,

"Wewe leo tunakukatakata."

Boga likajibu, "Wewe leo tutakukatakata."





Kweli, wakaanza kulikatakata. Lakini walishindwa. Ghafula akatokea mnyama mkubwa ajabu wa kushangaza kabisa ndani ya boga! Na jitu hilo linaitwa Shing'weng'we.

Nalo likaanza kuwameza watu wote pamoja na mifugo yao. Lilipomaliza kazi yake, likatokomea porini.

Akabaki mwanamke mmoja tu aliyekuwa na mimba. Yeye hakumezwa na Shing'weng'we, alijificha kwenye makapi ya mtama. Kutokana na yeye kubaki peke yake, vyakula vyote vilibaki kuwa vyake. Aliweza kula mpaka akanenepa mno.





Muda wake ulipotimia, alijifungua mtoto wa kiume, akampa jina la Masala Kulangwa (yaani ni mtu mwepesi kujifunza mambo). Kijana alipoanza kupata akili alimuuliza mama,

"Mama, mbona tuko wawili tu, wengine wako wapi?"

Mama alijibu, "Mwanangu, kua uyaone. Watu wote waliliwa na jitu moja liitwalo Lishing'weng'we. Tumebaki sisi wawili tu, mimi na wewe."

Lakini Masala Kulangwa aliposikia hayo, huzuni kubwa ikamjaa rohoni mwake. Tangu siku ile alikuwa na nia y kulikamata Lishing'weng'we na kuliua.

Mwishowe, mtoto huyo akawa kijana mkubwa. Akaanz kutembea peke yake. Siku moja, alipokwenda kucheza mbal vichakani, alimkamata panzi, na akarudi nyumbani huk akiimba kwa furaha kubwa wimbo wa kishujaa:

"Mama, mama nimemuua Shing'weng'we,
Amemaliza watu Shing'weng'we,
Mama, piga vigelegele,
Nimemuua Shing'weng'we,
Mama, piga vigelegele,
Nimemuua Shing'weng'we."

(mama hakupiga vigelegele, kwa kuwa Shing'weng'we alikuwa hajauawa).

Mama yake akamjibu, akamwambia, "Mwanangu huyu ni panzi tu, baba, siyo Shing'weng'we. Mlete hapa tumchome tumle."

Safari ya pili, aliua ndege Hondohondo (Dundo) akaja akiimba wimbo wake wa kishujaa.



"Mama mama nimemuua Shing'weng'we,
Amemaliza watu, Shing'weng'we, Mama, mama piga vigelegele,
Nimemuua Shing'weng'we."

(mama hakupiga vigelegele).

Mama akamwambia, "Mwanangu huyu ni ndege tu mkubwa. Tumnyonyoe

na kumchoma ili tumle, tumepata kitoweo."

Kijana aliendelea kufanya hivyo siku zote. Mwishowe, akawa kijana wa makamo.

Siku moja, Masala Kulangwa akaongea na mama yake, akamwambia, "Mama, nataka kuondoka nyumbani niende porini kutengeneza mishale ya kumuulia Shing'weng'we."

Mama yake alikubali na kijana alianza safari kuelekea msituni. Alipofika mbali kabisa na nyumbani, huku nyuma mama alianza kuimba wimbo ufuatao;

"Ninagongesha jiwe,
Ninagongesha jiwe."

Alipokuwa anaimba, jitu lile likasikia, likiwa porini. Likauliza na kuendelea kujibizana;

"Jiwe la kufanyia nini?"
"La kusagia mtama."
"Wa kula nani?"
"Wa kula na mwanangu."
"Amekwenda wapi?"
"Amekwenda msituni."
"Amekwenda kufanya nini?"
"Kutengeneza mishale."
"Ya kumchomea nani?"
"Ya kukuchoma na kukuua wewe."
"Nimekosa nini?"
"Umewameza watu wote."
"Mwache ajaribu, atakiona cha mtema kuni."

Hatimaye, kijana Masala Kulangwa akamaliza kutengeneza mishale yake, akarudi nyumbani akamwambia mama yake, "Mama, nimemaliza kutengeneza mishale, sasa naomba ruhusa niende kumtafuta Shing'weng'we, nimmalize."



Aliposikia hayo maneno, alihuzunika sana, alijishika shavu na kulalama, "Aaa! Mwanangu, utaliwezaje jitu la ajabu na la kutisha hivi? Maumbile yake ni makubwa mno, na kichwa chake ni cha ajabu. Mwanangu, usidhubutu kwenda! Mwanangu, acha kwenda; kaa nami. Hutaliweza."

Kijana akamjibu mamaye, akamwambia, "Mama, kwa nini niache kwenda? Kama siyo mimi, ni nani mwingine?" Mwanaume hujaribu, mwanaume hufia mbugani, mama."

Mwishowe, mama alikubali, "Kweli, wewe ni mtoto wa kiume. Sawa, basi nenda uendako, ukashinde vita hivyo. Nitakupatia chakula cha safari pamoja na baraka zangu."

Kijana akasema, "Na mimi pia nitakuachia ishara. Nitaweka maziwa mabichi mlangoni, yakiganda, ujue kwamba nimekufa. Na kama hayakuganda, ujue ni mzima bado."

Kwa hiyo, mama alimpa chakula mwanaye. Akambariki na kumpulizia maziwa kifuani na mgongoni, akisema, "Tembea salama na urudi salama, mwanangu."



Masala Kulangwa alibeba mishale yake na kile chakula cha safari (masurufu). Akaenda na baraka ya mamaye kumsaka Shing'weng'we.

Kwa siku tano alimsaka bila mafanikio. Ilipofika siku ya sita, akaita kwa sauti kubwa,

"Shing'weng'weeee! Shing'weng'weeee!

Shing'weng'we aliitikia kwa mbali kwa sauti kubwa ya kishindo cha kutikisa nchi, kama tetemeko vile. Alisema, "Niko hukuuu!! Niko mbali katikati ya nyika!" Shing'weng'we likauliza, "Ni nani wewe unayeniita?"

"Mimi Masala Kulangwa."

"Unaniitia nini?"

"Ninakuita tupigane nawe kwa kuwa umewamaliza watu wangu."

Masala Kulangwa akafuata kuelekea kule ilikotoka sauti. Akampata Shing'weng'we. Wakaonana ana kwa ana, akapigwa butwaa, akajiuliza, "Mungu wangu, sijui nitaliweza? Maskini mie." Alijikusanya kijana, akapiga moyo konde, akasonga mbele.

Alipokaribia, Shing'weng'we lilimuona na kumaka kwa dharau, "Mbilikimo, kinyangarika wewe, unatoka wapi na waenda wapi?"

Masala Kulangwa akasema, "Ninakutafuta wewe nikufutilie mbali kwa kuwa umewameza watu wote pamoja na mifugo yao."

Hapo Shing'weng'we kwa hasira aling'aka tena na kusema, "Njoo hapa, nikumeze nawe. Nitakufanya kuwa kitoweo cha ndege."

Masala Kulangwa alimjibu, "Mimi nipo, fanya kama utakavyo." Shing'weng'we akajibu, "Kama kweli uko tayari, tujenge kwanza jukwaa, halafu tuchome mawe saba ya moto ya kupigania."

Kila mmoja akatengeneza vijukwaa saba. Kijana akachoma mawe yake mpaka yakawa mekundu.

Na Shing'weng'we hali kadhalika, akafanya hivyo. Walipokamilisha, kila mmoja alipanda juu ya kijukwaa chake. Wakaambizana, haya tuanze sasa mapambano haraka, tuone nani atakayezidiwa nguvu. Mapambano makali yakaanza hatimaye. Ikawa piga kosa, piga kosa, hadi kila mmoja wao akabakiwa na jukwaa moja na jiwe moja.

Shing'weng'we akatupa jiwe lake la mwisho. Masala Kulangwa akakwepa. Zamu ya kijana kurusha jiwe lake la mwisho ikafika, akalirusha jiwe lake hilo *(ng'homango)* akamlenga katikati ya paji la uso, pa! Shing'weng'we akaanguka chini puu!!! Masala Kulangwa akakimbia mbio hadi alipo adui yake, akamwambia, "Leo rafiki ndiyo mwisho wako, umekufa."



Shing'weng'we akajibu, "Mmhh, ndiyo! Wewe kijana wangu, kweli mwanaume. Ama hakika wewe ni shujaa, yanipasa kukiri kuwa nimeshindwa. Lakini nikupe agizo moja, nikisha kufa, wakati wa kunichuna hakikisha unanichuna kuanzia mgongoni, siyo tumboni. Kwani ukinipasua tumbo, utakuwa umevimaliza vyote vilivyomo ndani."





Masala Kulangwa alichukua mishale yake akaanza kumchomachoma nayo kwa mfululizo. Shing'weng'we alishikwa na maumivu makali yasiyo kifani, akilia huku akikoroma. Shing'weng'we alipokata roho, Masala Kulangwa alichomoa kisu na kuanza kumchuna kuanzia mgongoni. Hapo watu wengi, wanaume kwa wanawake, watoto, wazee kwa vijana, pamoja na mifugo ya kila aina wakafumuka na kutoka nje ya tumbo la Shing'weng'we.

Kukawa na hoihoi, vifijo, nderemo na shangwe kubwa iliyokwenda sambamba na furaha na mshangao mkubwa. "Siku gani hii leo, tunaota au ni kweli.?" Masala Kulangwa aliwafariji na kusema, "Ndugu zangu, kamwe hiyo si ndoto, ninyi nyote mmetoka katika tumbo la Shing'weng'we, jitu la kutisha."

Mwishowe, mwenye chongo aliyetoka ndani ya tumbo la Shing'weng'we pia akawaambia watu, "Ninyi mna kiburi kabisa, mnasema ni ndoto, lakini hii siyo ndoto. Hamwoni damu na mifupa ya Shing'weng'we na hamtaki kukubali? Haya

ni maswali ya kijinga."

Watu wakaanza kurukaruka kwa furaha, wakamshukuru sana Masala Kulangwa. Wakasema, "Wewe ni mkombozi wetu na mfalme wetu wa dunia nzima. Masala Kulangwa oyeee!! Masala Kulangwa oyeee!!

Kijana akawaambia, "Leo ni siku ya furaha kwa watu wote. Haya mnifuate sasa ili nikamwarifu mama yangu aliyenisaidia kuupata ushindi huu." Masala Kulangwa aliendа huku anaimba wimbo wake wa kishujaa:

"Mama, mama, nimemuua Shing'weng'we,
Amemaliza watu, Shing'weng'we,
Mama, piga vigelegele.
Nimemuua Shing'weng'we."

Mama alipouona umati wa watu kwa mbali na mifugo yao wanaimba kwa sauti kubwa ya juu, akashikwa na mshangao akijiuliza, "kulikoni"! Mama huyo, alikimbia kwenda kuangalia maziwa mlangoni. Akakuta hayakuganda bado, akajisemea, 'mwanangu yuko hai' akakimbia kumpokea kwa furaha kubwa mno, huku akipiga vigelegele. Almanusura azimie huku akitokwa machozi ya furaha. Ilibidi watu wamsaidie mama huyo, "Pole sana mama, usije ukafa kwa furaha kubwa."

Maandamano makubwa ya wale waliokuwa wamekufa, walishangilia kwa wimbo;

"Mama, mwanao amefaulu kumua Shing'weng'we,
Mwanao amefaulu kututoa salama tumboni mwa Shing'weng'we,
Kweli umezaa simba anayenguruma, huyu ni mfalme wetu, Masala Kulangwa Oyeee! Oyeee!"

****



Kitabu hiki kinapatikana pia kwa

1. Kiingereza: Tears of Joy
2. Kisukuma: Shisoji ja Buyegi

Mathews Bookstores & Stationers
P.O. Box 42067
Dar es Salaam

ISBN 9987 602 39 8